# MTIHANI WA DARASA LA NNE MUHULA WA TATU 2017
# KISWAHILI

**Tumia vitenzi mwafaka kujazia vihasho 1 -15.**

Maembe ___1___ yalinunuliwa ___2___ hayajakomaa vizuri. Tulijaribu ___3___ sokoni . Lakini soko hilo ___4___ lilikuwa limefungwa ___5___ . Tulichukua ___6___ kikubwa, tukampa mama. ___7___ alituambia kuwa maembe ___8___ hayawezi kuoza ___9___ na kuwekwa pahali ___10___ .

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | mbichi | mibichi | mabichi | bichi |
| 2. | zikiwa | ikiwa | ukiwa | yakiwa |
| 3. | kuyarudisha | kuzirudisha | kuirudisha | kuvirudisha |
| 4. | nayo | nacho | nalo | naye |
| 5. | lote | yote | zote | chote |
| 6. | mfuko | gunia | debe | kikapu |
| 7. | hao | nayo | naye | nacho |
| 8. | zote | yote | lote | vyote |
| 9. | yakitunzwa | ikitunzwa | ukitunzwa | zikitunzwa |
| 10. | nzuri | mzuri | zuri | pazuri |

Maembe ni ___11___ sana mwaka ___12___. Miembe ___13___ imejaa ___14___ lakini bado ni ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | nyingi | mengi | vingi | mingi |
| 12. | hii | huyu | huu | haya |
| 13. | zote | yote | wote | lote |
| 14. | majani | mashina | bichi | mabichi |
| 15. | mbichi | mabichi | bichi | mabishi |

DAR 4 KISWAHILI

**Tumia jibu ni mwafaka kulingana na maagizo.**

16. Kitabu hiki ni changu. Kiashiria ni kipi
    A. kitabu  B. hiki
    C. ni  D. changu

17. Kanchiri pia ni ________
    A. bumbo  B. kasidiria
    C. sidiria  D. kizibao

18. Makao ya kuku ni ________
    A. mzinga  B. kizimba
    C. kombe  D. fuko

19. Kamilisha methali ifuatayo.
    Hasira ______
    A. hasira  B. asara
    C. hasara  D. hazara

20. Andika umoja wa :-
    Wageni wenu walituletea mikate tukala.
    A. mgeni wako alinileta mkate nikala.
    B. mgeni wake alinileta mkate nikala.
    C. mgeni wangu alinileta mkate nikala.
    D. mgeni wenu alituletea mkate tukala.

21. Nimenunua daftari
    A. mpya  B. jipya
    C. kipya  D. upya

22. Ukumbi wa kuwapokelea wageni au wa mazungumzo katika nyumba huitwa?
    A. Ukumbi  B. Sembule
    C. Sebule  D. Sebure

23. Wakulima ______ wanalima.
    A. wasita  B. sita
    C. watisa  D. wakumi


24. Neno lisiloambatana na mengine ni lipi?
    A. Tafadhali  B. Nipe
    C. Asante  D. Pole

25. Yupi si ndege wa nyumbani?
    A. Kuku  B. Kanga
    C. Bata  D. Bata mzinga

26. Tunachana nywele kwa kutumia ________
    A. kichana  B. kijana
    C. kitana  D. kichanuo

27. Chombo gani ni tofauti
    A. rununu  B. runinga
    C. bastola  D. tarakilishi

28. Taja umbo hili



    A. pia
    B. mche duara
    C. mche mstatili
    D. kopa

29. Mwalimu amebeba mipira ________
    A. mbili
    B. kubwa
    C. miwili
    D. nyeupe

30. **Andika wingi wa sentensi hii.**
    Goti linauma.
    A. goti zinauma.
    B. magoti yanauma
    C. goti yanauma.
    D. goti iinauma



Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31-40.

Ukoo ni watu wenye uhusiano wa karibu kama mama, baba, dada, kaka , babu, shangazi nakadhalika. Watu wa aila moja wanakuwa wa nasaba moja. Pia tunasema jamaa. Ukoo huwawezesha watu kuwa na utangamano mzuri na kusaidiana kimaoni. Hapo jadi watu wa ukoo mmoja hawakuruhusiwa kuoana na wakiona wangeadhibiwa vikali na wazee wa jamii hiyo.

31. Yupi si wa ukoo mmoja na baba
 A. babu
 B. dada
 C. mwalimu
 D. mama

32. Neno aila ni sawa na _____
 A. familia
 B. ukoo
 C. nasaba
 D. jamaa

33. Ukoo huleta ________
 A. utengano
 B. utangamano
 C. uvivu
 D. uhasama

34. Kuoana ni kufunga
 A. doa
 B. ndoa
 C. toa
 D. zoa

35. Lipi halifai
 A. ukoo
 B. nasaba
 C. jamii
 D. aila

36. Hapo jadi ni
 A. samani
 B. zamani
 C. chadi
 D. juzi

37. Tunasema damu nzito kuliko
 A. ukoo  B. maji
 C. mafuta  D. ngeu

38. Mtoto wa mwana ni
 A. mjukuu
 B. kitukuu
 C. mjomba
 D. mkaza mwana

39. Watu wa ukoo mmoja hawakuruhusiwa
 A. kutangamana
 B. kutembea
 C. kuoana
 D. kuketi pamoja

40. Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni?
 A. Ukoo
 B. Koo
 C. Jamii
 D. Hapo jadi



Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

**Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41- 50.**

Shule ya Bidii,
S.L.P 201 - 9403,
NAIROBI.
JULAI ,18, 2016.
} P

Kwa rafiki Kadzo.
Pokea salamu chekwa kutoka kwangu. Nina uhakika kama mauti kuwa u mzima mithili ya chuma cha poa. Je, unapasipasi shuleni au unanoanoa?
Madhumuni ya kukuandikia waraka huu ni kukujulisha kuwa shule tutafunga Agosti 14, tutakapofunga shule nitakujulia hali hapo mjini Buraha. Tutacheza pamoja na watoto wengine wanaoishi humo mtaani

Wako wa Mtimani,
Chanda pete.

41. Barua hii ni ya _______
   A. kindugu   B. kidugu
   C. kidungu   D. kindungu

42. Sehemu " P" huitwa _______
   A. anwani   B. kimalizo
   C. tarehe   D. rafiki

43. Mwandishi ni _________
   A. Buraha
   B. Kadzo
   C. Chanda pete
   D. Shule

44. Barua hii iliandikwa muhula wa
   A. kwanza   B. pili
   C. tatu   D. Hatujaambiwa

45. Neno chekwa lina maana
   A. kwa ufupi   B. kwa wingi
   C. vizuri   D. kwa kawaida

46. Kinyume cha kupasa ni
   A. upasipasi   B. kufeli
   C. kurudi   D. kulala

47. Mpokezi wa barua aliishi
   A. Buraha   B. Kadzo
   C. Chengoni   D. Hatujaambiwa

48. Madhumuni ni
   A. lengo   B. fedha
   C. kiwango   D. ni vyema

49. Barua ni nusu ya
   A. kuandika
   B. kuonana
   C. kucheka
   D. kusoma

50. Jina lingine la barua ni _______
   A. waraka   B. karatasi
   C. nyenzo   D. maandisho



Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com